




MUHTASARI WA MODULI YA MFUMO SHIRIKISHI WA UHAKIKI (PGS)

Umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ulioandaliwa na TOAM kwa kushirikiana na wadau wa PGS Tanzania



MAANDALIZI YA MAARIFA HAYA

- Nakala hii ni tafsiri ya kiswahili ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) uliotengenezwa awali kwa lugha ya Kiingereza kupitia ushirikiano wa shirika la kilimohai Tanzania (TOAM) na IFOAM – Organics International.
- Mwongozo huo ulishirikisha wadau wa PGS nchini Tanzania kuchangia ujuzi na maarifa ya namna mfumo huu unapaswa kutekelezwa.
- Kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki (KHEA), TOAM iliweza kutafsiri mwongozo wa mafunzo haya kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha matumizi yake kwa wadau mbali mbali wa mnyororo wa thamani. iliunga mkono tafsiri ya mwongozo huu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, kama sehemu ya kuwezesha upatikanaji na usambazaji wa maarifa kuhusu PGS.

UTANGULIZI KUHUSU MAARIFA HAYA

- Mwongozo huu wa Mafunzo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) ni sehemu ya mfululizo wa nyenzo za mafunzo unaojumuisha **moduli tano**, zilizolenga kuwajengea washiriki uelewa na uwezo wa kutumia Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS) katika Kilimohai.
- Nakala hii imejikita katika moduli 5 inayoangazia dhana ya masoko na fursa mbalimbali zilizopo katika kilimohai kwa ajili ya uendelevu wa PGS.
- Nakala nyingine za mafunzo kwa ajili ya moduli zilizotangulia zinapatikana kama sehemu ya mfululizo huu, hivyo watumiaji wanashauriwa kuzitumia kwa pamoja ili kupata maudhui kamili ya mafunzo ya PGS.

MODULI YA TANO

Masoko katika Mfumo Shirikishi wa Uhakiki (PGS)

Muhimu: Seti hii ya nakala za mafunzo kwa moduli ya 1-5 inapaswa kutumika kwa kufuata mwongozo wa Mtaala wa Mafunzo ya PGS kwa Wawezeshaji (ToT), 2025

Masoko katika PGS

Yaliyomo:

- Malengo ya kujifunza
- Uuzaji wa Bidhaa za Kilimohai kutoka Vikundi vya PGS Vilivyoimarika
- Zoezi la 1 kwenye Kutambua Fursa za Masoko kwa Vikundi vya PGS
- Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii
- Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Kuimarisha utendaji wa PGS



Masoko katika PGS...



Malengo ya kujifunza:

- Kuwawezesha washiriki kuelewa dhana ya masoko katika mfumo wa PGS.
- Kufafanua nafasi ya wanachama wa PGS katika kufanikisha malengo ya masoko ya kikundi na kuhakikisha uendelevu wa mfumo wa PGS.

Masoko katika PGS...

1. Kujenga Soko Imara la Bidhaa za Kilimohai

Lengo mojawapo la PGS ni kujenga soko la uhakika la bidhaa za Kilimohai. Soko zuri linapaswa:

- **Kufikika** kwa urahisi kwa wazalishaji na walaji.
- Kuwa na bidhaa za kutosha na zenye **ubora unaohitajika**.
- Kuwezesha bei **zinazokubalika** kwa wazalishaji na wanunuzi kwa wakati mwafaka



Masoko katika PGS...

Uhamasishaji wa Masoko

(Ukiongozwa na TOAM/Wadau wengine, kwa ushirikiano na vikundi vya PGS)

Katika ngazi ya PGS, shughuli za uhamasishaji wa masoko zinapaswa kujumuisha:

- Kutambua na kulenga makundi muhimu ya watumiaji na wanunuzi.
- Kuelewa mahitaji ya walaji.
- Kuandaa ujumbe unaofaa na kuchagua njia sahihi za kuwafikia walaji.
- Kuelimisha jamii kuhusu Kilimohai na nembo ya Kilimohai.



2. Kupanga Uzalishaji Kulingana na Mahitaji ya Soko

Mipango mizuri ya uzalishaji husaidia kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa kwa wakati na kujenga imani kwa wanunuzi.

Shughuli Muhimu:

- Chagua mazao au bidhaa za kulima na kuuza kwa Pamoja.
- Fuatilia nani analima nini na kwa kiasi gani.
- Fuatilia ratiba za mavuno ili kuhakikisha upatikanaji.
- Toa uhakikisho wa uidhinishaji wa Kilimohai kwa watumiaji na umma.
- Tangaza kazi ya kikundi ili zifahamike na kuvutia wanunuzi.

3. Kubadili tabia za walaji ili kuunga mkono masoko ya kilimohai

Lengo ni kuwahamasisha walaji:

- Kuchagua bidhaa za Kilimohai badala ya bidhaa za nyingine.
- Kutambua na kuthamini thamani ya bidhaa za Kilimohai.
- Kuendelea kununua bidhaa za Kilimohai mara kwa mara.

Shughuli za Kufanikisha ushawishi

- Kutoa elimu kuhusu faida za Kilimohai.
- Kushiriki maonesho na kampeni za uhamasishaji
- Kutumia ushuhuda wa wakulima na walaji



4. Kupanga Njia za Masoko na Usambazaji wa Bidhaa

Hii inahusu jinsi bidhaa na huduma zinavyosafirishwa kutoka kwa mzalishaji hadi kwa mlaji

- **Bidhaa:** Bidhaa za Kilimohai
- **Huduma: Usafirishaji,** Uuzaji, Ukusanyaji wa bidhaa kutoka kwa wakulima n.k.
- **Watoa huduma:** Wakulima, Vikundi vya wazalishaji, Watoa huduma za usafirishaji na ugavi



Mambo Muhimu katika Kusimamia Masoko

- Kutafuta masoko ya uhakika.
- Kupanga taratibu za usafirishaji wa bidhaa.
- Kuweka bei inayofaa.
- Kuweka mfumo wa Kupokea maoni kutoka kwa walaji.
- Kuweka utaratibu wa Kushughulikia changamoto za walaji na wanunuzi.



Zoezi la 1: Kutambua Fursa za Masoko kwa Vikundi vya PGS

Lengo:

Kutambua masoko yaliyopo na fursa mpya za masoko kwa bidhaa za Kilimohai.



Zoezi la 1...

Sehemu ya 1: Majadiliano

Lengo: Kutambua namna ya kutumia masoko yaliyopo na kuanzisha masoko mapya ya bidhaa za Kilimohai.

Mambo ya kujadili

1. Masoko yaliyopo katika eneo lenu.
2. Changamoto za kufikia masoko hayo.
3. Njia za kuboresha upatikanaji wa masoko.
4. Kushirikishana uzoefu wa mafanikio na changamoto za masoko.

Muda: Dakika 15-20

Zoezi la 1...

Sehemu ya 2: Kazi ya Vikundi (Watu 3–5 kwa Kila Kikundi)

Lengo: Kuandaa mpango wa masoko unaoendana na mahitaji ya kikundi chenu cha PGS. Majadiliano hayo yanaweza zingatia mojawapo ya maeneo haya:

- Kutumia fursa katika masoko yaliyopo ya bidhaa za Kilimohai: Orodhesha na tathmini masoko yaliyopo kulingana na eneo husika
- Kuanzisha masoko mapya: Jadili njia za Kuanzisha Masoko Mapya ya bidhaa za kilimohai

Matokeo ya majadiliano: Kila kikundi kiwasilishe mpango wake wa masoko katika kikao cha pamoja.

40 - 45 minutes

Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii

Majadiliano

Kwa nini uendelevu ni muhimu katika uendeshaji wa PGS?

PGS endelevu huhakikisha:

- Uhai na ufanisi wa mfumo kwa muda mrefu.
- Umiliki wa mfumo na wanajamii wenyewe.
- Manufaa endelevu kwa wadau wote wanaohusika.



Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii...

Miongozo Muhimu ya Kufanikisha Uendelevu

- 1. Dira ya Pamoja: Kujitolea katika kudumisha maadili, malengo ya pamoja ya PGS.**
- 2. Umiliki na mshikamano wa Jamii :** Kuimarisha uongozi wa ndani, ushiriki wa wanachama na maamuzi ya pamoja ili kuendeleza shughuli za PGS.



Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii...

Miongozo Muhimu ya Kufanikisha Uendelevu..

3. Uwazi na uendelevu wa huduma za Kifedha

- Kuweka wazi gharama zinazohitajika na kutumika.
- Kuandaa utaratibu wa kuchangia gharama kupunguza utegemezi wa ufadhili wa nje.



Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii...

Miongozo Muhimu ya Kufanikisha Uendelevu...



4. Msaada Endelevu kwa Wakulima

- Kutoa msaada wa mafunzo mara kwa mara
- Kuwezesha upatikanaji wa masoko (kama maeneo ya masoko ya wakulima)
- Kukuza na kutangaza bidhaa za Kilimohai kwa walaji
- Kushirikishana taarifa za masoko (mfano bei za bidhaa na mwenendo wa mahitaji ya soko).

Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii...

Miongozo Muhimu ya Kufanikisha Uendelevu...

5. Kujifunza kwa pamoja na kujengeana uwezo

- Kuandaa mafunzo ya rejea kila mwaka ya kuhuisha ujuzi ili kuimarisha uelewa na utekelezaji wa PGS.
- Kuhamasisha ziara za mafunzo na kubadilishana uzoefu kati ya vikundi vya PGS ili kukuza uelewa na ubunifu.



Uendelevu wa PGS katika Ngazi ya Jamii...

Miongozo Muhimu ya Kufanikisha Uendelevu...

6. Kuimarisha Msaada wa Kitaasisi

- Kuimarisha huduma zinazotolewa na TOAM kwa kuhamasishaji wa uanachama hai na ushiriki wa wanachama katika shughuli mbalimbali.



Matumizi ya Teknolojia ya Kidijitali katika PGS

Lengo la Kujifunza:

Kuelewa jinsi teknolojia za kidijitali zinavyoweza kusaidia kuhifadhi, kusimamia na kusambaza taarifa za PGS na kuwezesha ufuatiliaji wa bidhaa kwa uwazi zaidi.



-

Matumizi ya Teknolojia ya Kidijitali katika PGS...

Matumizi ya Msimbo wa QR katika PGS

- Kuhifadhi taarifa muhimu za mkulima, mazao, uthibitishaji na ripoti.
- Kuwezesha walaji kutumia simu janja kuskani na kupata taarifa za bidhaa kwa urahisi.
- Kurahisisha ufuatiliaji ili kuongeza uwazi na kuimarisha imani ya walaji.



Matumizi ya Teknolojia ya Kidijitali katika PGS...

Mjadala: Manufaa ya Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika PGS

1. Je, ni faida gani za kutumia misimbo ya QR na KoboToolbox katika usimamizi wa taarifa za PGS?
2. KoboToolbox inawezaje kuharakisha ukusanyaji wa taarifa na kupunguza hatari ya kupotea kwa kumbukumbu muhimu?
3. Ni aina gani za taarifa zinazopaswa kuhifadhiwa katika mfumo wa kidijitali wa PGS?

Matumizi ya Teknolojia ya Kidijitali katika PGS...

Mjadala: Utekelezaji wa Zana za Kidijitali katika Vikundi vya PGS

- Je, wanachama wa kikundi wanahitaji kujengewa uwezo katika maeneo gani?
- Je, ni mafunzo gani ambayo wanachama wanayahitaji ili kutumia misimbo ya QR na *Kobo Toolbox* kwa ufanisi?



Hatua Zinazofuata Baada ya Mafunzo

1. Kushirikishana Uzoefu wa Mafunzo (Tathmini ya Mafunzo).
2. Kujaza fomu ya tathimini binafsi baada ya mafunzo

Seti hii ya slaidi za mafunzo kwa wakufunzi (ToTs) za Moduli 1–5 inapaswa kutumika sambamba na miongozo iliyotolewa katika Mwongozo wa Mtaala wa Uendelezaji wa PGS kwa Mafunzo ya Wakufunzi (ToT), 2025.

HITIMISHO

- Hii ni Moduli ya 5 na ya mwisho katika mfululizo wa mafunzo ya PGS.
- Maarifa yaliyopatikana katika moduli zote tano yanapaswa kutumika kwa pamoja katika kuimarisha uelewa, utekelezaji na maendeleo ya Mfumo Shirikishi wa Uhakiki katika jamii.

Asante kwa kushiriki katika mfululizo huu wa mafunzo.

Tunawatakia mafanikio katika kutumia maarifa haya katika kuimarisha PGS na Kilimohai nchini Tanzania.

*Imeandaliwa na Shirika Mwamvuli la Kilimohai Tanzania
(TOAM) kupitia mradi wa kitovu cha maarifa Afrika Mashariki
(Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology
Tanzania - KHEA)*

Kupata moduli nyingine tembelea jukwaa la kidijitali la maarifa ya
Kilimohai na kilimoikolojia katika tovuti: <https://khea-africa.org/>

Tunapatikana:

Mtaa wa Samora Avenue, Jengo la Kelvin House, gorofa ya Kwanza.
Kwa mawasiliano Zaidi tupigie kupitia +25574413499